



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TANGAZO LA MWALIKO WA TAASISI NA ASASI ZA KIRAIA ZENYE NIA  
YA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA KATIKA UCHAGUZI MDOGO WA  
UBUNGE JIMBO LA ISMANI, HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA NA  
MADIWANI KATIKA KATA 12 ZA TANZANIA BARA**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Ismani lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Mkoa wa Iringa na Madiwani katika kata 12 za Tanzania Bara. Uchaguzi huo utafanyika siku ya Jumatatu tarehe 01 Juni, 2026 katika Jimbo tajwa na kata zifuatazo:-

Na.	Halmashauri	Kata
1.	Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni	Mzimuni
2.	Halmashauri ya Manispaa ya Kahama	Zongomera
3.	Halmashauri ya Mji Nzega	Itilo
4.	Halmashauri ya Mji Tarime	Ketare
5.	Halmashauri ya Mji Kasulu	Nyumbigwa
6.	Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi	Kala
7.	Halmashauri ya Wilaya ya Igunga	Ziba
8.	Halmashauri ya Wilaya ya Mlele	Kamsisi
9.	Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe	Nyamugali
10.	Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru	Namasakata
11.	Halmashauri ya Wilaya ya Chato	Bwongera
12.	Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti	Kibiti



Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 10(1)(g) na (h) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 292, kikisomwa pamoja na kanuni ya 22 na 23 za Kanuni za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi za Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatoa mwaliko kwa taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura katika uchaguzi nchini.

Hivyo, kupitia tangazo hili, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inakaribisha maombi kutoka kwa taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu hiyo.

Taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura zinatakiwa kuwasilisha maombi yao kupitia kiunganishi (*link*) ifuatayo <https://ams.inec.go.tz> katika Mfumo wa Kusajili Waangalizi, Asasi za Kiraia na Vyombo vya Habari (Accreditation Management System - AMS).

Taasisi au asasi ya kiraia itakayoomba inatakiwa kuwa na vigezo vifuatavyo:-

- (i) iwe imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;
- (ii) iwe imefanya kazi nchini kwa kipindi kisichopungua miezi sita tangu kusajiliwa kwake;
- (iii) ikiwa taasisi au asasi ya kiraia inahusisha watendaji wa kimataifa, miongoni mwa watendaji wake wakuu watatu, wawili wawe Watanzania;
- (iv) katika utendaji wake, iwe haijahusishwa na uchochezi au kuvuruga amani;
- (v) iwe na uzoefu wa kutoa elimu ya mpiga kura; na
- (vi) iwe tayari kujigharamia katika kutoa elimu ya mpiga kura.

Aidha, taasisi au asasi ya kiraia itakapowasilisha maombi katika mfumo, inatakiwa kutekeleza yafuatayo:-

- (i) kuambatisha nakala au kivuli cha cheti cha usajili;
- (ii) kuambatisha nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika;
- (iii) kujaza majina matatu ya viongozi wa juu wa taasisi au asasi husika; na
- (iv) kujaza anuani kamili ya makazi na namba za simu za ofisi na za viongozi wake.

Maombi hayo yatapokelewa kuanzia tarehe 21 Aprili, 2026 hadi 27 Aprili, 2026.



Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa ajili ya kugharamia zoezi la utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa taasisi au asasi za kiraia zitakazopewa kibali.

Aidha, maombi yatakayotumwa kwa njia tofauti na mfumo ulioainishwa katika tangazo hili hayatafanyiwa kazi.

Limetolewa leo tarehe 20 Aprili, 2026 na:



Kaillma, R. K

MKURUGENZI WA UCHAGUZI

